



## TANGAZO KWA UMMA

### KANUNI MPYA ZA BIASHARA YA KUBADILISHA FEDHA ZA KIGENI

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuutaarifu Umma kuwa Kanuni za Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni (*Foreign Exchange [Bureau de Change] Regulations, 2019*) zimetolewa na zinapatikana katika tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania ([www.bot.go.tz](http://www.bot.go.tz)). Aidha, Kanuni hizi zilichapishwa katika gazeti la Serikali lenye Na. 450 mnamo tarehe 7 Juni 2019.

Benki Kuu ya Tanzania pia inapenda kuutaarifu Umma kuwa Kanuni za Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni ya 2015 (*Foreign Exchange [Bureau de Change] Regulations, 2015*) zimefutwa rasmi na hazitumiki tena.

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**21 JUNI 2019**